

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME
SHULE YA SEKONDARI KIBACHA, S.L.P 149, SAME

TAREHE: 07/12/2020

KUMB. Na KSS/JI/2021

NDUGU:

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Napenda kukarifu kuwa umechguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Kibacha. **HONGERA SANA**. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 siku ya Jumatatu. Siku hiyo ndiyo utasajiliwa. Ukichelewa zaidi ya siku tano bila sababu na taarifa kwa Mkuu wa Shule hutapokelewa tena.

SARE: Sare ya shule ni shati jeupe la mikono mifupi kwa wanafunzi wote, suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana rangi ya **damu ya mzee** na viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi na vya kufunga kwa kamba. Upana wasuruali ni inchi 18, urefu ni kugusa viatu na sketi ipite chini ya magoti. Wasichana waislamu watavaa hijabu ndefu rangi nyeupe.

MAHITAJI YA KITAALUMA: Daftari kaunta 9, rula, mathematical set, kalamu, na penseli yenye ufuto. Kamusi ya Kiingereza, iliyoandikwa: **OXFORD STUDENT'S LEARNING DICTIONARY, 3RD EDITION**. Ratiba ya Shule kila siku: Saa 01:00 asubuhi – 10:00 jioni

MAHITAJI YA USAFI: Wanafunzi wote waje na mafagio aina ya chelewa. Wavulana waje na jembe jipya lenye mpini, wasichana waje na ndoo ya lita 20.

AFYA: Kila mwanafunzi awasilishe hati ya kuthibitisha afya yake kutoka kwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya kwa kujaza fomu iliyoambatishwa nyuma ya maelekezo haya.

MUHIMU: Kila mwanafunzi lazima aletwe shuleni na mzazi au mlezi wake wakati wa usajili. Mwanafunzi aje na form hii siku ya usajili. Siku ya usajili wanafunzi watapata maelekezo kuhusu sheria, kanuni, nidhamu, utamaduni wa shule na makosa ambayo yanaweza kumfukuzisha mwanafunzi shule.

Nakutakia safari njema unapojiunga na shule hii. Hutajuta kujiunga na shule hii ukitambua kilichokuleta.

.....
OMARY MAGONGO

(MKUU WA SHULE)

(0784-348226)

